TANGAZO LA SERIKLAI N0 41 LA TAREHE 28/04/2006

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7,(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU)ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI , 2016.

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika.	1	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi (Ada na UShuru)za mwaka 2016 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali
Matumizi	2.	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.
Tafsiri	3	Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-
		"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma,vibali,au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.
		"Afisa Muidhiniwa" maana yake Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
		"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu,watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni,au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

“Kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashuri kutekeleza au kusimamia jambo au kazi husika.

“Kituo cha Mabasi” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia au kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

“Machinjio” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

“Maegesho” maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

“Masoko” maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

“Mnada” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Usajili wa vyombo vya usafiri” maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

“Wakala” maana yake ni Mtu,Taasisi,Kampuni,au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

“Pombe ya asili” maana yake ni pombe zinazotengenezwa na kuzalishwa ndani ya jamii ya Mufindi zikiwa na majina yanayojumuisha ingawa sio lazima komoni,dezeli, wanzuki,kimpumu,mbege na ulanzi.

“Stakabadhi ya malipo” maana yake ni stakabadhi maalumu itolewayo na Halmashauri baada ya malipo ikijulikana kama

HW5 na yenye nembo ya Halmashauri.

"Madini ya Ujenzi" itakuwa na maana ya aina zote za Miamba, Mawe, Udongo wa mfinyanzi, Changarawe, Mchanga, Tofali, Kokoto na mengineyo.

"Mitaa" maana yake ni njia, barabara au eneo ambapo Halmashuri inaweza kuliainisha kuwa eneo la maegesho.

"Maegesho ya hifadhi" maana yake ni maegesho yaliyotengwa

SEHEMU YA II

ADA NA USHURU MBALIMBALI

Ushuru wa Madini ya Ujenzi

4 Halmashauri itatoza Ushuru wa Madini ya Ujenzi kutoka kwa wanunuzi wa madini hayo ndani ya Mamlaka ya Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

Maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini

5 (1) Halmashauri itatenga na kuainisha maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi

(2) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuchimba madini ya ujenzi bila kibali cha Halmashauri.

(3) Mchimbaji yoyote wa madini ya Ujenzi atatakiwa kuzingatia Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika kuchimba madini hayo.

(4) Ushuru wa madini utalipiwa wakati gari linapotoka katika eneo yanapochimbwa na kuandaliwa madini hayo au katika vizuizi vya Halmashauri.

Msamaha wa Ushuru wa Madini ya Ujenzi

6 (1) Halmashauri inaweza kuruhusu madini kuchimbwa na kusombwa bila kulipiwa ushuru kwa kibali maalum kitakachotolewa na Mkurugenzi.

Ushuru wa Maegesho

7 (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa kila gari litakaloegeshwa kwenye maeneo ya kuegesha magari kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Saba la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru wa maegesho wa magari unaweza kulipwa kwa siku/saa au kwa mwezi na utalipwa baada ya gari kuegeshwa.

(3) Halmashauri itaainisha maeneo katika mitaa kuwa ni sehemu ya maegesho yaliyohifadhiwa.

Gari Iliyotelekezwa

8 (1) Gari itahesabika imetelekezwa ikiwa itafungwa mnyororo kwa zaidi ya masaa matatu (3) bila kulipiwa ambapo baada ya muda huo litapelekwa kwenye karakana ya Halmashauri na likikaa kwenye karakana ya Halmashauri kwa muda zaidi ya siku kumi na nne(14) bila kukombolewa na baada ya muda huo Halmashauri itaomba kibali katika Mahakama kuuza gari hilo na kufiia gharama katika mnada wa hadhara.

Msamaha wa Maegesho

9 (1) Magari yafuatayo yatasamehewa kulipiwa ushuru wa maegesho chini ya Sheria Ndogo hizi;

a) Magari ya Wagonjwa(Ambulance)
b) Magari ya Serikali na Taasisi zake
c) Magari ya Majeshi
d) Magari ya Zimamoto.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (1) Halmashauri inaweza kusamehe gari lolote kulipiwa ushuru wa maegesho endapo itaridhika na sababu atakazotoa muombaji wa msamaha.

SEHEMU YA III

MAANA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

10 (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru kwa ajili ya shughuli mbalimbali zinazoendeshwa na wananchi ndani ya Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza mpaka Jedwali la Kumi na Mbili kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Ada na Ushuru utozwao na Halmashauri utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

11 (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa 12 kamili asubuhi mpaka saa 1 kamili jioni au muda wowote ule bidhaa au mizigo itakapopitishwa katika mageti au vizuizi vya kukusanyia Ada na Ushuru yaliyowekwa na Halmashauri.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa katika ya Halmashauri/Wakala na mlipa Ada na Ushuru.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Uteuzi wa Wakala

12 Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, Kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

13 Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

a) Kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;
b) Kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia mashartui ya mkataba wa uwakala;
c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla yakusaini Mkataba.
d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unaohusika na Mkataba wake.
e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha Uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano(5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala kwa kila mwezi;
f) Kumchukulia hatua za Kisheria mtu yoyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

SEHEMU YA VI

MAKOSA NA ADHABU

Makosa **14** Itakuwa ni kosa kwa;

(1)Kwa wakala;

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au Mkataba kutoka kwa Halmashauri;

(b) Atajaribu au atakusanya Ada na Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika Mkataba;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa hasara aliyosababisha na atatozwa faini ya Shilingi Mia Mbili Elfu(200,000/=) au kifungo cha miezi Sita(6) jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2)Kwa mtu yeyote ambaye;

a) Atashindwa,atadharau,atapuuza,au atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

b) Atamshawishi mtu au kikundi cha watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

c) Atatengeneza,atatayarisha,ataidhinisha utengenezaji,au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri,au atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

e) Atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu,au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;Na

f) Atamzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja(100,000/=) au atatumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili(12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani fani na kifungo.

Kufifisha **15** Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua

Kosa		Shilingi Elfu Hamsini(50,000/=) na isiyozidi Shilingi Laki Tatu(300,000/=)kwa kosa iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Kumi na Moja la Sheria Ndogo hizi.
Tangazo la Serikali Na. 41/2005 na Tangazo la Serikali Na.255/2008	**16**	Sheria Ndogo hizi inafuta Sheria Ndogo(Ada na Ushuru)za Mwaka 2006 na 2008 ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

YAMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 10(1)

JEDWALI LAKWANZA

1. Ada ya Matangazo ya biashara

	Aina ya Tangazo	Kiwango cha Ushuru
i.	Maombi ya kuweka mabango ya Biashara/kuchora	Shs. 10,000/=
ii.	Matangazo yanayong'aa(yanayowaka kwa nguvu ya umeme) Kwa mitaya mraba kwa mwezi	Shs. 30,000/=
iii.	Ubao wa tangazo usioangaza kwa mita ya mraba	Shs.30,000/= kwa mwezi
iv.	Kodi ya pango(kwa mabango au mbao zisizo za matangazo)	Shs.20,000/= kwa mwezi
v.	Bango la Tangazo lisiloangaza (kwa mita ya mraba)	Shs. 50,000/= kwa mwezi
vi.	Bango laTangazo linaloangaza (kwa mita ya mraba)	Shs.90,000/= kwa mwezi
vii.	Tangazo kwa kutumia Kitambaa	Shs. 60,000/= kwa siku
viii.	Tangazo la Karatasi	
	(a) Ukubwa wa A4	Shs. 1,000/= kwa siku
	(b) Ukubwa wa A3	Shs. 1,200/= kwa siku
	(c) Ukubwa wa zaidi ya A3	Shs. 1,500/= kwa siku
ix.	Matangazo ya Ukutani kwa mita za mraba	Shs.70,000/=kwa mwezi
x.	Tangazo kwa kutumia vyombo vya usafiri na vipaza sauti	Shs.10,000/=mwezi
xi.	Bango la Tangazao linalobadilikabadilika	Shs. 200,000/= Kwa mwaka
xii.	Matangazo kwa njia ya maonyesho	
	(a) Kutambulisha bidhaa	Shs.5,000/= kwa saa
	(b) Kutambulisha huduma	Shs. 3,500/= kwa siku

JEDWALI LA PILI

2. Ada ya kukodi Mali za Halmashauri

(i)	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe	Shs.250,000/=kwa siku
(ii)	Ukumbi wa Ofisi za Ujenzi	Shs. 100,000/=kwa siku
(iii)	Ukumbi wa Ofisi za Kilimo	Shs 100,000/= kwa siku

(iv) Kukodi viti/meza — Shs. 500/= kwa kiti/meza
(v) Mitambo(trekta,vifaa vya GPS,Projector n.k. — Malipo kwa mkataba.

Ada na Ushuru wa vibanda vya biashara

(a) Katika masoko (kwa soko/eneo) — Shs.15,000/= kwa mwezi
(b) Maeneo ya mengine ya Wilaya — Shs.10,000/= kwa mwezi

JEDWALI LA TATU

---

3. Ada na Ushuru wa Soko na Minada

Ada na Ushuru wa Sokoni kwa meza……Shs. 300/= kwa siku

(i) Ada na Ushuru wa Minada

(a) Meza…… Shs.1,000/= kwa siku
(b) Wauza mitumba/nguo,vyombo,urembo,spea,viatu Shs. 1,000/= kwa siku
(c) Mamalishe…….Shs. 1,000/= kwa siku
(d) Vinywaji……Shs. 2,000/= kwa siku
(e) Biashara ndogondogo……Shs. 500/= kwa siku
(f) Pombe za Asili…… Shs. 1,000/= kwa siku

(ii) Ada na Ushuru wa Mnada/Minada ya Mifugo;

(a) Ushuru wa Ng'ombe…… Shs. 3,000/= kwa ng'ombe
(b) Ushuru Mbuzi,Kondoo,Nguruwe…… Shs. 2,000/= kwa kila mmoja
(c) Kuku/Kanga/Bata/Njiwa…….Shs. 1,000/=kwa tenga moja

(iii) Jedwali la Orodha ya Minada na tarehe inayofanyika ndani ya Halmashauri;

Na.	MNADA	KIJIJI	KATA	TAREHE YA MNADA
1.	Malangali	Tambalang'ombe	Malangali	Kila tarehe 25 ya kila mwezi
2.	Lugodalutali	Igombavanu	Igombavanu	Tarehe…….ya kila mwezi

(iv) Jedwali la Orodha ya Magulio na tarehe yanayofanyika ndani ya Halmashauri;

Na.	GULIO	KIJIJI	KATA	TAREHE YA GULIO
1	UGESA	UGESA	IHALIMBA	KILA TAREHE 5 YA KILA MWEZI
2	MGOLOLO	MABAONI	MAKUNGU	KILA JUMAMOSI YA TATU YA MWEZ
3	MTAMBULA	NYAKIPAMBO	MTAMBULA	KILA JUMAMOSI YA TATU
4	MBALAMAZIWA	NYANYEMBE	M/MAZIWA	KILA JUMAMOSI YA PILI
5	SADANI	SADANI	T/NG'OMBE	KILA TAREHE 21 YA MWEZI
6	UGENZA	UGENZA	IKWEHA	KILA TAREHE 27
7	KIBAO	KIBAO	MTWANGO	KILA JUMAPILI YA KWANZA
8	IHOWANZA	IHOWANZA	IHOWANZA	KILA TAREHE 1
9	NYOLOLO	NYOLOLO	NYOLOLO	KILA TAREHE 20
10	MDABULO	KIDETE	MDABULO	KILA JUMAPILI YA PILI

JEDWALI LA NNE

4. Ada na Ushuruwa mazao mchanganyiko

(a) Viazi…… 3%ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(b) Kabichi…….3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(c) Karoti……...3% ya bei ya shamba kwa guia la debe sita
(d) Ufuta……..5% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(e) Kahawa…….. 5% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(f) Mchele……..3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(g) Maharage…….3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(h) Vitunguu saumu……3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(i) Vitunguu maji…….3% ya bei shamba kwa gunia la debe sita
(j) Nyanya……..3% ya bei ya shamba kwa tenga moja
(k) Mahindi/Alzeti/Ngao/Mtama……3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita
(l) Mazao mengine yasiyotajwa…….3% ya bei ya shamba kwa gunia la debe sita

JEDWALI LA TANO

5. Ada ya huduma ya machinjio,Ukaguzi wa nyama na Ushuru wa Bucha

(a) Ng'ombe……..Shs. 2,500/= kwa kila mmoja atakayechinjwa
(b) Kondoo,Mbuzi na Nguruwe……Shs. 1,800/= kwa kila mmoja atakayechinjwa
(c) Kuuza na kuchoma Nyama mnadani …….Shs. 1,500/= kwa siku
(d) Ushuru wa Bucha la Ng'ombe,Mbuzi,Kondoo,Nguruwe na Samaki……Shs. 500/= kwa siku

JEDWALI LA SITA

6. Ada ya kuendesha shughuli za utamaduni na michezo

(a) Ada ya kuendesha shughuli za Muziki na Michezo

(i) Kibali cha kuchezesha disko……..Shs. 30,000/= kwa siku moja
(ii) Kibali kwa ajili ya sherehe…….Shs. 30,000/- kwa siku
(iii) Kibali cha kuchezesha michezo mingine……..Shs. 60,000/= kwa mwezi

(b) Ada ya uzalishaji wa pombe za asili

(i) Uzalishaji kwenye viwanda vidogodogo……..Shs. 30,000/= kwa mwezi
(ii) Uzalishaji kwa mtu mmoja mmoja……Shs. 1,000/= kwa kibali kimoja

JEDWALI LA SABA

7. Ada na Ushuru wa Stendi,Maegesho na Usajili wa vyombo vya usafiri

(a) Ada na Ushuru wa Maegesho ya vyombo vya usafiri.

i. Pikipiki ……Shs. ……kwa siku
ii. Teksi……..Shs…….kwa siku
iii. Lori chini ya Tani 2/Pick up……..…Shs……kwa siku
iv. Lori chini ya Tani 5/Fuso……..Shs…….kwa siku

v. Lori zaidi ya Tani 5……..Shs…….kwa siku
vi. Magari mengine yasiyo ya biashara…….Shs……kwa siku

(b)**Ada na Ushuru wa stendi**

i. Baiskeli……Shs……..kwa kutoka
ii. Pikipiki…….Shs……kwa kutoka
iii. Teksi/Gari chini ya abiria 5……Shs….. kwa kutoka
iv. Basi chini ya abiria 25…….Shs. 500 kwa kutoka
v. Basi zaidi ya abiria 25……Shs. 1,000/= kwa kutoka
vi. Basi zaidi ya abiria 40……Shs. 2,000/= kwa kutoka

JEDWALI LA NANE

---

8. Ada na Ushuru wa madini ya Ujenzi

1.	Mchanga/Vifusi	Tshs 3,500/- kwa tripu kwa ujazo wa 1-3.3m Tshs 5,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 3.4-4.8m Tshs 8,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 4.9m na kuendelea
2.	Mawe	Tshs 3,500/= kwa tripu kwa ujazo wa 1-3.3m Tshs 5,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 3.4-4.8m Tshs 8,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 4.9m na kuendelea
3.	Kokoto	Tshs 3,500/= kwa tripu kwa ujazo wa 1-3.3m Tshs 5,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 3.4-4.8m Tshs 8,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 4.9m na kuendelea
4.	Tofali	Tshs 3,500/= kwa tripu kwa ujazo wa 1-3.3m Tshs 5,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 3.4-4.8m Tshs 8,000/= kwa tripu kwa ujazo wa 4.9m na kuendelea

JEDWALI LA TISA

VIBALI VYA UJENZI

9. Ada na tozo za vibali vya ujenzi

1) Viwanja vya makazi…….Shs. 40,000/=
2) Taasisi mbalimbali (shule, vyuo, ofisi n.k.)……Shs. 200,000/=
3) Viwanda vikubwa vya uzalishaji……..Shs. 200,000/=
4) Viwanda vidogo…….Shs. 100,000/=
5) Vituo vya mafuata…….…….Shs. 200,000/=
6) Uzio/fesnsi ya Tofali……..…….Shs. 20,000/=
7) Uwanja wa michezo,hotel za utalii
   ambazo sio ghorofa …….……..Shs. 150,000/=
8) Ghorofa 1 hadi 4 ……..…..Shs. 200,000/=
9) Zaidi ya ghorofa 5……..……Shs. 500,000/=
10) Minara ya simu……..…….Shs. 200,000/=
11) Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapo juu……Shs. 20,000/=

JEDWALI LA KUMI

10. Ada ya huduma za Burudani mpya

1) Wamiliki wa kumbi mbalimbali…….Shs. 50,000/= kwa siku
2) Wapambaji wa kumbi za burudani(harusi,kitchen party,
   sherehe za kuaga binti/kijana n.k…….Shs. 50,000/= kwa siku
3) Watoa huduma za chakula kwenye sherehe……Shs. 50,000/= kwa malipo ya siku
4) Mshereheshaji(MC)…….Shs. 20,000/= kwa siku
5) Mtoa huduma ya muziki……Shs. 20,000/= kwa siku
6) Mtoa huduma ya picha na video…….Shs. 20,000/= kwa siku

JEDWALI LA KUMI NA MOJA

HATI YA KUKIRI KOSA
(Chini ya Kifungu cha 14)

Mimi……nakiri mbele ya ……..……ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mufindi, kwamba mnamo tarehe ……..ya mwezi…….mwaka…….nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha …….cha sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi za mwaka 2016. Nipo tayari kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi atatekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Saini ya mtenda kosa:…….

Mbele ya;

Jina:…….

Saini:……

Wadhifa:…….

Tarehe …….

JEDWALI LA KUMI NA MBILI

FOMU YA KUFIFISHA KOSA

(Chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi…….wa
S.L.P……..

Nanayefanya biashara ya……katika eneo la…….

Lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.Nakiri kuwa leo tarehe…….

Nilikiuka kifungu cha ……Sheria Ndogo za(Ada na Ushuru)za Halmashauri yaWilaya ya Mufindi za mwaka 2016.Kwa hiyo,kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yoyote,nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya Kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ya mtenda kosa:……

Mbele ya;

Jina:…….

Saini:……

Wadhifa:…….

Lakiri na Mhuri wa Halmshauri ya wilaya ya Mufindi umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani ulioitishwa na kufanyika tarehe …….. ya mwezi ……. 2016 na imebandikwa mbele ya :-

.....
DR. RIZIKI SHEMDOE
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

.....
MH. FESTO MGINA
MWENYEKITI HALMASHAURI,
WILAYA YA MUFINDI

NAKUBALI,

George B. Simbachawene (Mb)

WAZIRI WA NCHI-OR-TAMISEMI

DODOMA

TAREHE……..…2016.